HOTUBA YA JAJI MKUU MHE. PROF. IBRAHIM HAMIS JUMA YA UFUNGUZI WA MKUTANO WA BARAZA KUU LA WAFANYAKAZI WA MAHAKAMA YA TANZANIA KATIKA UKUMBI WA LAPF

TAREHE 29, JUNI, 2022 JIJINI DODOMA

Wahe. Majaji wa Mahakama ya Rufani mliopo,

Mhe. Jaji Mustapher Siyani, Jaji Kiongozi,

Mhe. Jaji Gerson Mdemu, Jaji Mfawidhi Dodoma,

Wahe. Majaji Wafawidhi,

Wahe. Majaji wa Mahakama Kuu mliopo,

Mhe. Mtendaji Mkuu wa Mahakama,

Mhe. Msajili Mkuu wa Mahakama,

Katibu wa Baraza,

Makamishna wa Tume ya Utumishi wa Mahakama,

Viongozi wengine wa ngazi mbalimbali wa Mahakama na Tume,

Viongozi toka TUGHE Makao Makuu na Mkoa,

Ndugu Waandishi wa Habari,

Mabibi na Mabwana;

Nawassalimu kwa jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania....

Ndugu Wajumbe,

Baada ya Salaam, naomba kuchukua fursa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwenye kustahili sifa zote, kwa kutuwezesha sote kusafiri salama na kufika hapa Dodoma kutoka maeneo yetu mbali mbali nchini. Napenda kuchukua fursa hii kuwakaribisha katika Mkutano huu muhimu wa BARAZA LA WAFANYAKAZI WA MAHAKAMA YA TANZANIA.

Vile vile nawashukuru viongozi wote wa mabaraza ya wafanyakazi wa Mahakama ngazi ya Kanda na Mikoa ambayo mmeweza kufanya vikao vya mabaraza hayo na hatimaye sasa kushiriki kikamilifu katika BARAZA HILI KUU LA KITAIFA la Mhimili wa Mahakama.

Kipekee Namshukuru pia Mhe. Mustapher Mohammed Siyani (Jaji Kiongozi) ambaye ameshiriki baadhi ya Mikutano ya Kanda na kutoa ufafanuzi wa baadhi ya mambo ambayo yalijiri ngazi ya Kanda.

Ndugu Wajumbe na wageni waalikwa,

Mkutano huu wa Baraza umewekwa kwa mujibu wa Sheria ili kuwapa wajumbe wa Baraza nafasi kupitia na kujadili kwa kina masuala mbalimbali muhimu yanayohusu utekelezaji wa majukumu ya msingi ya Mahakama. Napenda pia niwashukuru wale wote walioshiriki katika maandalizi ya Mkutano huu Muhimu.

Wote mnafahamu wajibu wa Msingi wa Mhimili wa Mahakama ni utoaji haki katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Moja ya sababu kubwa ya mkutano huu ni kutathmini, kujitathmini na kuainisha mikakati ya kuboresha utendaji wetu katika kuhakikisha kuwa Haki inatolewa na inapatikana kwa wakati na kwa ueledi wa hali ya juu bila vikwazo visivyokuwa na sababu ya msingi.

Ndugu Wajumbe,

Kama ambavyo wengi wenu mnafahamu Baraza la Wafanyakazi ni jukwaa muhimu sana la kuwashirikisha wafanyakazi katika utekelezaji wa wajibu muhimu wa utoaji haki katika sehemu zetu za kazi. Kwa vyovyote vile hakuna haki bila wajibu kwa hiyo tuna

kazi kubwa kuhakikisha kuwa hata wale wanaohitaji haki tunawasaidia na kuwaelimisha kuhusu wajibu wao kufuata sheria na taratibu za kupata Haki. Huu wajibu ni kwa wateja wa ndani (watumishi) na wateja wa nje (yaani wadau wetu).

Umuhimu wa Baraza hili umekuwa ukionekana kila Mwaka kwa ushiriki wa watumishi kuleta chachu ya maendeleo yetu na ufanisi katika utoaji haki. Tutaendelea kuboresha ufanisi wa Mikutano hii ya Baraza ngazi ya Taifa, na tutaimarisha mikutano ya Kanda ili kuhakikisha kuwa kikao cha Kitaifa kinakuwa na maoni na mapendekezo yanayotoka kuanzia ngazi ya Mahakama za Mwanzo. Kimsingi katika Baraza ngazi ya Taifa, itapendeza zaidi kupokea changamoto ambazo zimewashinda viongozi wa Kanda ambao wanafanya kazi kwa niaba ya MAHAKAMA Makao Makuu.

Kuwepo kwa viongozi za TUGHE ngazi ya Mkoa na Taifa ni kuwezesha pia kupata maoni kutoka kwa hawa wadau wetu ambao, ingawa wao sio sehemu ya utumishi wa Mahakama, ila ni sehemu muhimu tunapozungumzia Haki za Watumishi wa Mahakama na za Watanzania kwa ujumla.

Ninawasihi wafanyakazi wote wa Mahakama kupitia nyie wajumbe wa Baraza, na wadau wote katika mnyororo wa haki, jitambueni kuwa jukumu la utoaji haki ni sehemu muhimu ya maendeleo ya nchi yetu na watu wake. Utekelezaji wa Wajibu wenu katika utoaji haki unaimarisha utawala wa sheria na pia utawala bora.

Utekelezaji wa Wajibu wenu unachangia pia uwepo wa amani ya nchi, na huimarisha uchumi na ustawi wa Watanzania. Kila Mtumishi wa Mahakama atambue kuwa yeye ni sehemu ya mnyororo wa utoaji haki. Unapotimiza wajibu wako kikamilifu na kwa uadilifu, mnyororo wa Haki unakuwa imara na kufanikisha uwekezaji na pia shughuli za biashara za ndani na za kimataifa.

Hata watalii wanaongezeka kutokana na kazi nzuri ya Mhe. Samia Suluhu Hassan kupitia mkakati wa 'Royal Tour', wanafurahia kuja Tanzania kutokana na kuwepo kwa amani ambayo inatokana na watumishi waadilifu katika mnyororo wa utoaji Haki.

Ndugu wajumbe wa Baraza na wageni waalikwa,

Nawapongeza wafanyakazi wote wa Mahakama kwa kufanikisha utekelezaji wa Mpango Mkakati na Programu ya Maboresho. Hii ni

miongozo endelevu katika shughuli zetu za kila siku. Ni lazima kwa viongozi, watumishi na wajumbe wote wa Baraza kuyaelewa kwa kina, yote yaliyomo katika programu za maboresho na mpango mkakati.

Kila mtumishi wa Mahakama inabidi afahamu mwelekeo na dira ya Mahakama. Wajumbe hamna budi kuendelea kuwaelimisha watumishi wote wapi Mahakama ya Tanzania inapoelekea. Tusipofanya hivyo tutakuwa kama *wachezaji wa mpira wa Miguu ambao hawajui goli lao la kufunga na kwamba kuna wakati wanaweza kujifunga hata wenyewe.*

Kwa muktadha huo upo umuhimu wa Wafanyakazi wote na wadau kufahamu Muundo wa Mahakama, Kanuni za Utumishi, Kanuni za Fedha na masuala ambayo yako ndani ya uwezo wa uongozi wa Mahakama, na mambo ambayo yako nje ya uwezo wa uongozi wa Mahakama.

Mfano masuala ya Mishahara, Maslahi, Bajeti na hata Rasilimali watu, Mahakama inategemea sana mipango ya Mhimili wa Serikali. Hata hivyo nitumie fursa hii kuishukuru Serikali

inayoongozwa na Mhe. Samia Suluhu Hassan kwa jinsi inavyotuwezesha kwa hali na mali na ambavyo inatoa kipaumbele kwa mahitaji ya Mhimili wa Mahakama. Ukisema MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA MWAKA 2022-23 utaona namna Serikali inavyojitahidi kuimarisha miunda mbinu ya Mahakama.

(1) Ujenzi wa Majengo ya Mahakama za Wilaya.
(2) Ujenzi wa upanuzi wa jengo la chou cha Uongozi wa Mahakama – IJA.
(3) Ujenzi na ukarabati wa majengo ya Mahakama za Mwanzo.
(4) Ukarabati wa jengo la Mahakama Kuu Tabora.
(5) Nyumba za Majaji na Mahakimu.
(6) Ujenzi wa Vituo Jumuishi.
(7) Ujenzi wa Makao Makuu Dodoma.

Ndugu Wajumbe na wageni waalikwa,

Hivi karibuni Serikali ya Tanzania imechukua tena Mkopo wa gharama nafuu wa dola za Kimarekani milioni 90 (zaidi ya Bilioni Tsh 210) kwa ajili ya kuimarisha miundo mbinu ya Mahakama Tanzania kwa mwaka ujao wa Fedha 2022/23.

Nimetaarifiwa na Mtendaji Mkuu wa Mahakama, kwamba hata kwa miradi ya maendeleo inayoendelea sasa MAHAKAMA, Wizara ya Fedha imekuwa ikitoa fedha kwa wakati na hata pale ambapo kuna changamoto yeyote, mawasiliano yanafanyika kwa haraka.

Nitumia fursa hii kipekee kumshukuru Waziri wa Fedha, Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba na Katibu Mkuu Wizara ya Fedha Bw. Emmanuel Tutuba kwa ushirikiano wao wa hali ya juu kuhusu upatikanaji wa fedha. Ninawaomba waendelee kutuunga mkono na sisi Mahakama tutaendelea kusimamia vizuri matumizi ya fedha za Umma.

Wafanyakazi na Watumishi, nawaomba tuhakikishe tunatimiza wajibu wetu kuhakikisha kuwa Mkopo Serikali ya Tanzania iliyochukuwa kutoka Benki ya Dunia inatumika kusogeza utoaji haki kwa Watanzania kwa miaka mingi ijayo.

Ujumbe wa Benki ya Dunia utawasili nchini kuja kuangalia namna tunavyokamilisha Programu ya Kwanza ya Maboresho, na namna tulivyojitayarisha kutumia Mkopo ambao umetolewa. Tuwape ushirikiano wa kutosha na tuwaonyeshe kuwa kweli

tunausimamia na kuutekeleza mradi kwa matarajio ya Serikali ya Tanzania na Benki ya Dunia.

Pengine ni vyema mkafahamu kuwa katika jitihada za kuhakikisha mfumo matumizi ya fedha ni imara, nimejulishwa kuwa, katika ujenzi wa vile Vituo 6 Jumuishi, baada ya vipimo vya mwisho *(re-measurement)*, tumeweza kuokoa zaidi ya Bilioni Tsh 3.5. Fedha zilizobakizwa kwenye ujenzi zimetumika kununulia vitendea kazi vingine ambavyo vitazidi kumarisha ufanisi wetu katika utoaji haki.

Nawapongeza wote waliofanikisha uhakiki, wakiongozwa na Mkuu wa Kitengo cha Maboresho (Naibu Msajili Dkt. Angelo Rumisha) huo na kuokoa fedha hizo na kutumia katika shughuli zingine. Ni matumani yangu awamu ya pili tutaokoa fedha nyingi zaidi na tutafanya mambo mengi zaidi.

Ndugu Wajumbe,

Mwaka jana, Tume ya Utumishi wa Mahakama ilitunga Kanuni kadhaa kuhusu uendeshaji wa Mahakama ambazo zinawagusa watumishi. Kanuni hizi ni Pamoja na—

Judiciary Administration (General) Regulations, 2021 (Tangazo la Serikali Namba 1 la 2021); *Judiciary Administration (Internal Finance) Regulations, 2020* (Tangazo la Serikali Namba 2 la 2021); *Judiciary Administration (Service Scheme), 2021* (Tangazo la Serikali Namba 2 la 2021).

Watumishi tujenge utamaduni wa kuzimiliki hizi kanuni zetu tuzielewe na zitusaidie kutoa huduma. Ni watumishi wachache mno ambao wanafahamu namna kanuni hizi zinafanya kazi. Ni wajibu wa Viongozi kuhakikisha kuwa watumishi wanaelewa namna Kanuni zinazotumika kuendesha shughuli za Mahakama na zinavyowagusa katika utoaji wa huduma. Uelewa wa watumishi kuhusu Kanuni utasaidia sana kufanya kazi iwe nyepesi kwani tutakuwa tunaongea lugha moja yenye ufahamu na uelewa mmoja kwa wakati mmoja.

Ni wajibu wa Viongozi kuhakikisha kuwa watumishi wanaelewa namna Kanuni zinazotumika kuendesha shughuli za Mahakama na zinavyowagusa katika utoaji wa huduma. Uelewa wa watumishi kuhusu Kanuni utasaidia sana kufanya kazi iwe nyepesi kwani tutakuwa tunaongea lugha moja yenye ufahamu na uelewa mmoja

kwa wakati mmoja. Viongozi wa Makao Makuu, Kanda, Divisheni, Mikoa na Wilaya tujenge utamaduni wa kujibu hoja za watumishi kwa uwazi na ukweli. Tusisubiri hoja zijibiwe kwenye Baraza Kuu ilihali majibu wa Kanuni za Utumishi na Fedha zipo chini ya usimamizi wenu.

Ndugu wajumbe na wageni waalikwa;

Naomba sasa mniruhusu, baada ya kueleza haya mambo ya jumla nizungumze japo kwa kifupi juu ya maeneo mahsusi **manne** kabla ya kumaliza hotuba yangu;

(i) TEHAMA

Ndugu wajumbe,

Dunia imezidi kuwa kama Kijiji (tena huenda imefikia hatua ya kuwa kitongoji, na siku zijazo itakuwa kama mtaa tu). Kasi ya mabadiliko ya Teknolojia, inaongezeka kwa kasi kubwa sana na hakuna anayeweza kubashiri tutaishia wapi. Kama mnavyofahamu Serikali imewekeza sana katika ujenzi wa miundombinu ya TEHAMA.

Wafanyakazi wote wa Mahakama ya Tanzania, na wadau wetu, tusikubali kubaki nje ya Mradi Mkubwa wa Serikali ukiwepo mradi mkubwa uitwao TANZANIA YA KIDIJITI *(Tanzania Digital Project)* iliyoanza mwaka jana (2021).

Mradi huu unasisitiza azma ya Serikali ya Tanzania kutumia teknolojia na mitandao kufanikisha shughuli za kiuchumi na kijamiii katika zama hizi za Mapinduzi ya Kidijiti. Mtakumbuka WIKI na SIKU YA SHERIA (Januari na Februari, 2022) Mahakama iliweka wazi azma yake ya kuanza safari ya kufikia MAHAKAMA MTANDAO.

Ndugu Wafanyakazi, naomba nisisitize kuwa safari ya kuhamia MAHAKAMA MTANDAO au MAHAKAMA YA KIDIJITI inahitaji matayarisho na mabadiliko ya TABIA, UTOAJI HUDUMA, marekebisho ya sheria, kanuni, taratibu na hata namna tulivyozoea kutoa huduma.

Nafahamu wajibu wa Muajiri wa kuwatayarisha na kuweka programu za mafunzo endelevu ambayo yatawawezesha wafanyakazi wa kada zote kuhama kutoka utoaji huduma kwa njia

zilizozowekwa hadi kutoa huduma katika Mahakama ya Kidijiti au Mahakama Mtandao. Kila Mfanyakazi wa Mahakama atapata mafunzo maalum yatakayompa, angalau ujuzi wa awali wa kidijiti *(Basic Digital Skills)*.

Natoa wito kwa Mtendaji Mkuu wa Mahakama, Msajili Mkuu na Mkuu wa Chuo cha Uongozi wa Mahakama (IJA), kutafakari mafunzo maalum. Chuo kitathmini mitaala yake ya sasa ili ijumuishe mafunzo ya ngazi mbali mbali za KIDIJITI.

Ndugu Wajumbe na Wageni waalikwa;

SERIKALI inapozungumza safari ya TANZANIA YA KIDIJITI, na kwamba huduma kwa umma zitatolewa kidijiti, ni wakati pia kwa watumishi wote wa Mahakama na wadau wa mfumo mzima wa utoaji haki kuanza kuzinduka, kujichambua na kujitathmini utayari wao wa kuhama kifikra.

Kwa watumishi wote wa Mahakama ni wakati wa kuchambua hatua zilizo mbele ya safari yetu na changamoto zote zitakazoweza kujitokeza katika mpango mzima wa safari ya kwenda MAHAKAMA MTANDAO/KIDIJITI kwa ngazi zote za mahakama.

Ni wakati wa viongozi wa Mahakama katika Kanda, Divisheni, na Makao Makuu; kupima utayari wa kila mtumishi kuhamia MAHAKAMA MTANDAO/KIDIJITI *(Digital Migration)*. Huu pia ni wakati wa kupanga mambo ya kufanywa wakati wa mpito *(transition period)* kutoka Mahakama za Kawaida *(Manual)* hadi mahakama mtandao endelevu.

Hapa naomba niwakumbushe kuwa ndio maana hata kwa nafasi zaidi ya 200 kwa ajili ya ajira mpya, usaili wa kwanza ulifanyika kwa njia ya mtandao ili kila atakayeajiriwa, hata awe dereva, awe na mawazo ya kufanya kazi kidijiti.

Kwa kutumia TEHAMA pia tuliweza kuchambua maombi zaidi ya 15,000 ndani ya masaa 24 na kuwapata wale waliotakiwa kuja kufanya usaili wa awali na kwamba hao waliofanya usaili walifanya kwenye mikoa mbali mbali na majibu ya usaili wa kimtandao, majibu yalikuwa yakipatikana mara mtahiniwa anapomaliza kujibu maswali kwa muda aliopangiwa, ambao nao ulipangwa kidijiti.

Kuthibitisha faida ya TEHEMA kwa kutumia mfano huu halisi wa usaili, mchakato ulianza tarehe 15 Juni, 2022 na kufikia siku ya Jumatano tarehe 22 Juni, 2022 tulishajua majibu na uchambuzi ulikuwa rahisi na wa kisayansi kwa sababu ya matumizi ya TEHAMA.

Ndugu Wajumbe;

Katika kuhamia MAHAKAMA MTANDAO/KIDIJITI *(Digital Migration),* usalama wa nyaraka za kimahakama na za utoaji haki ni mambo yanayohitaji kujitayarisha kwa kina. Wakati wa mpito ni wakati wa kutathmini usalama wa nyaraka za kimahakama; kutathmini Menejimenti ya Mashauri; kutathmini ufanisi wa upatikanaji wa taarifa za Mahakama na kutathmini nafasi ya wadau wa Mahakama katika safari ya MAHAKAMA MTANDAO.

Aidha, wakati wa mpito kuelekea Mahakama ya Kidijiti ni wakati wa kuainisha hatua zote ambazo masuala ya haki yatapitia KIDIJITI ndani ya mifumo ya wadau mbali mbali mbali katika mnyororo wa utoaji haki hadi kuingia ndani ya ngazi mbali mbali za Mahakama. Kwa ufupi, hakuna uwezekano wa kufanikisha Safari ya Mahakama Mtandao au Mahakama ya Kidijiti bila

mabadiliko ya dhati ya kifikra, kiutamaduni na kiutendaji kwa watumishi wote wa Mahakama.

Ili kufikia Mahakama Mtandao ya Kweli na imara; **ni muhimu sasa Ofisi ya Mtendaji Mkuu wa Mahakama kwa kushirikiana na Ofisi ya Msajili Mkuu wa Mahakama kuweka mkakati mpana wa kuwezesha mabadiliko haya ya Kifikra na kiutendaji kwa watumishi wetu wote bila kujali umri, kada, cheo, au kiwango cha elimu** (Hapa naomba nirudie).

Ndugu wajumbe na waalikwa wote;

Katika kutekeleza hili hata maeneo ya pembezoni yapewe kipaumbele na siyo maeneo ya mijini tu. Ni muhimu sote tuwe kwenye safari moja na asiwepo atakayeachwa nyuma eti kwa kuwa yuko kwenye Mahakama ya maeneo ya vijijini.

Itapendeza hata yale maeneo ambayo ni maalum kwamba ni vigumu kufika *(Hard to reach areas)*, kama *NANJILINJI (Kilwa-Lindi), LUKUMBULE (Tunduru – Ruvuma), MWIMBI (Kalambo – Rukwa), KINUSI (Mpwapwa – Dodoma), HAUBI (Kondoa – Dodoma) n.k*, tunapojenga majengo ya Mahakama, tufikirie jinsi ya

kuwafikia kwa miundombinu ya Mtandao. TEKNOLOJIA na MAHAKAMA MTANDAO ndio itayageuza maeneo yasiyofikika yawe ya kufikika.

Itapendeza kwa mfano kesi ikiwa Mahakama ya Mwanzo Nanjilinji, Wilaya ya Kilwa Mkoa wa Lindi, halafu kwa njia ya *video conference,* Hakimu aliyeko Mahakama ya Mwanzo itakayojengwa Ilangala, Wilaya ya Ukerewe Mkoa wa Mwanza anaisikiliza kesi hiyo.

Huko ndiko tunakotaka kufika na ni watumishi wa Mahakama ndio mtatufikisha huko!! Jambo muhimu ni kwamba sote tuwe na nia hiyo na tuwe na Imani hiyo na tuhakikishe hatusimami bali tunaelekea huko tunakotaka kwenda na sio kwingineko. Mwanafalsafa Dkt. Martin Luther King Junior aliwahi kusema; Ninanukuu

'Kama huwezi kupaa, kimbia, kama huwezi kukimbia, tembea, kama huwezi kutembea angalau tambaa na kwamba hakikisha kuwa kwa vyovyote vile upo kwenye mwendo.'

Kwa falsafa hii ni Imani yangu kuwa sisi Mahakama wakati wote tutakuwa tunakimbia ili wanaotembea, wajifunze kutoka kwetu natusiwe wachoyo kuwashirikisha wadau wetu mikakati yetu ili nao waongeze mwendo.

(ii) Maslahi na mambo yanyohusu watumishi

Ndugu wajumbe,

Nafahamu wazi kuwa zipo changamoto mbalimbali ambazo zinawakabili katika kutekeleza majukumu yenu ya kikazi. Nina taarifa kuwa ofisi ya Mtendaji Mkuu inaendelea kushughulilia changamoto mbali mbali na huwa ananipatia taarifa.

Niwahakikishie kuwa Ofisi yangu inafuatilia kwa karibu kupata taarifa ya utatuzi wa changamoto mbalimbali. Hata hivyo ni muhimu sana kufahamu kuwa changamoto zingine, zinatatuliwa na mhimili mwingine na ni vyema kuvuta subira.

Ninafahamu kuwa Mtendaji Mkuu kwenye taarifa yake na mazungumzo yake atafafanua mengi kwa kina ukizingatia kuwa mengine yameshajadiliwa kwenye ngazi ya Kanda na kupatiwa

ufumbuzi. Baadhi ya mambo ambayo nafahamu yanashughulikiwa ni pamoja na;

(a) Upandishwaji wa madaraja kwa Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo wasio na Shahada ya Sheria *(PCMs)* ambao wamekwama kwa muda mrefu.

(b) Uboreshaji wa maslahi ya watumishi

(c) Vyombo vya usafiri

(d) Upatikanaji wa vitendea kazi vya kutosha kama kompyuta

(e) Bajeti kuwa finyu

(f) Kuchelewa kubadilishiwa Kada na kupandishwa madaraja

(g) n.k

Ndugu Wajumbe,

Ninyi mlipo hapa ni wawakilishe wa watumishi zaidi ya 5,500 wa Mahakama Tanzania, naomba muamimi kwamba Uongozi wa MAHAKAMA unafanya jitihada kuwa kupata ufumbuzi wa changamoto mbali mbali ambazo mnakabiliana nazo.

Ni imani yangu kuwa MAHAKAMA itazidi kuwa sehemu bora ya kufanyia kazi na kisima cha ‘ubunifu’. Wito wangu kwenu ni kuendelea kuchapa kazi kwa uadilifu na kwa pamoja tuijenge MAHAKAMA.

Pamoja na kwamba ni haki ya Mtumishi kuhama taasisi ya Umma kwa kufuata utaratibu, bado mimi nashangaa wanaofikiria kuwa waondoke MAHAKAMA kwa sasa waende sehemu yenye maslahi mazuri, ila naamini maslahi yetu yakishakuwa bora watatamani tena kurudi.

Watu kama hao sio watumishi bali ni wafanyakazi na wanachoangalia wao ni maslahi yao sio Maslahi ya Umma na Taasisi. Mtendaji Mkuu amenijulisha kuwa alikuwa akiwaruhusu (hasa *Non- judicial Officer*) kwa kuwa ni haki yao kisheria ila naye amekuwa akiwaambia hao wanaoharakisha kuhama kuwa wajiulize wanamuachia nani Mahakama kuiboresha?.

(iii) Wafanyakazi wajiongezee Maarifa kwa ajili ya kutoa Huduma Bora kwenye karne inayoongozwa na TEHEMA

Ndugu wajumbe, Viongozi na wageni waalikwa;

Karne ya 21, ambayo inatawaliwa na Teknolojia inayosukumwa na Mapinduzi ya Nne ya Viwanda, ni Karne ya "JAMII YA MAARIFA" *(Knowledge Society)*. JAMII YA MAARIFA inajengwa na kile kinachotajwa katika moja ya Malengo Matano ya Dira ya Maendeleo ya Taifa—***"kuwepo jamii iliyoelimika vyema na inayojifunza."*** Maarifa mengi hayawezi kukufuata wewe Mfanyakazi mmoja mmoja.

Hakuna kiwango cha mafunzo ambacho muajiri wako, chuo chochote duniani au hata Serikali inaweza kukupa wewe mtumishi ili uwe na Maarifa ya kutosha kufanya kazi katika JAMII YA MAARIFA INAYOBADILIKA KILA WAKATI.

Kinachotakiwa kutoka kwa kila Mtumishi wa Mahakama, na kila Mtanzania, kuchukua hatua binafsi, bila kujali kama utapata msaada kutoka kwa wengine, kutambua mahitaji yako ya kuongeza maarifa, kujiwekea malengo binafsi ya kujitafutia

maarifa yote unayohitaji, kujiainishia nyenzo za kupata hayo maarifa. Kwa ufupi, jukumu la kutafuta maarifa kukuwezesha kuwa mtumishi bora wa Mahakama ni jukumu lako binafsi na ni jukumu endelevu kwa vile hakuna wakati Maarifa hutosha.

Ndugu wajumbe;

Sisi viongozi wenu tunawahakikishia kuwa kwa kadri rasilimali fedha itakavyoruhusu tutawasaidia wale wote ambao wao wenyewe wana nia na ari ya kujiendeleza. Tutajitahidi kuwatafutia ufadhili kusoma katika maeneo ya kimaboresho kwa mfano ujuzi na maarifa kufanya kazi katika MAHAKAMA MTANDAO.

Hata mwajiri anapokupa ruhusa ya kuhudhuria mafunzo kwa kujilipia bado amekupa mchango mkubwa sana. Utakapohitimu, cheti kitaandikwa jina lako lakini elimu na maarifa yatakuwa na msaada mkubwa kwa utoaji haki.

Kwa wale ambao wako karibu na vyuo vya elimu ya Juu vinayotoa masomo ya jioni ni vyema sana kuanza kuchangamkia fursa hii kuanzia Majaji, Mahakimu, watendaji na watumishi saidizi *(supporting staff)*. Jitahidini kuchukua masomo

yatakayowawezesha kufanya kazi na kutoa huduma kwa ufanisi kulingana na mahitaji ya zama za Mapinduzi ya Nne ya Viwanda. Chukueni masomo yatakayowawezesha kuendelea kuhitajika hata pale Mapinduzi ya Nne ya Viwanda yanaleta mabadiliko na mahitaji mapya.

Usikubali kubakia na kiwango cha maarifa, ujuzi ulioupata kutoka elimu na mafunzo yenye maudhui ya Karne zilizopita. Watumishi wenye kazi za Kihakimu *(Judicial Officers)* kama Majaji na Mahakimu, mjitahidi kutafuta ujuzi, maarifa kutoka taaluma zingine ambazo zitawaboresha katika kutoa huduma, kwa mfano TEKNOLOJIA.

Hivyo hivyo, watumishi saidizi *(supporting staff)* tafuteni elimu na maarifa ya kuboresha utoaji wenu wa huduma na hata kuwawezesha kufanya kazi zaidi ya moja kwa wakati mmoja. Ni muhimu sana ieleweke kuwa sizungumzii watumishi wa Makao Makuu tu, bali ni watumishi wa Mahakama Nchi nzima.

Ndugu wajumbe na wageni waalikwa;

Kuna kosa kubwa ambalo sisi watumishi hufanya, kufikiria kiwango cha elimu yako kinachoonyeshwa katika vyeti ni kielelezo kuwa una maarifa ya kutosha kukabiliana na changamoto za dunia ya kidigiti.

Kuna kosa pia kudhani, kufanya kazi kwa mazoea ya muda mrefu tunakuwa na maarifa ya kutosha kukabiliana na maboresho au mabadiliko makubwa yanayosukumwa na teknolojia. Unaweza kabisa ukapata bahati ya kujiongeza na kupata shahada ya Uzamili au Uzamivu, lakini ukawa bado huna maarifa ya kujiongeza kila siku kukuwezesha kutoa huduma ya utoaji haki inayotakiwa katika Karne ya 21.

Kipimo cha huduma sio shahada uliyo nayo bali ubora wa huduma inayopimwa kila siku. Kuna tofauti ya kusoma na kupata cheti na kusoma na kuelimika ili utumie elimu yako kutatua changamoto. *Hatutakumbukwa kwa sababu ya viwango vya elimu yetu bali mchango wetu katika kutatua changamoto kwa kutumia elimu zetu.* Ndio maana kuna msemo wa Kichina unaomaanisha kwa Kiswahili kwamba;

Haijalishi kwamba Paka ni mweusi au mweupe, madam anakamata Panya, huyo ni paka (*It doesn't matter whether a cat is black or White, provided it chatches mice it is a cat!*)

Maadamu ukiweza kutatua tatizo, hutaulizwa ulipata GPA ya ngapi? Ukitoa huduma bora utachukuliwa kuwa wewe ni mtumishi bora wa MAHAKAMA.

Hazina ya maarifa kukuwezesha kufanya kazi katika mazingira yanayobadilika kila wakati ni kujifunza na kujitafutia maarifa ya kimaboresho kila siku na kujazia maarifa ya kimazoea uliyonayo tayari ili uweze kutatua changamoto za wateja wengi kwa muda mfupi na kwa ueledi wa hali ya juu.

Ndugu wajumbe na Wageni waalikwa;

Karne ya 21 ya Mapinduzi ya Nne ya Viwanda inayo maarifa mengi na ujuzi mwingi unaotusubiri kujiendeleza na kufikia. Kila siku, watumishi tunatakiwa kujiuliza kuhusu maarifa mapya ya kutafuta kuboresha huduma za utoaji haki. Teknolojia ndio eneo ambalo limebeba maarifa mapya ambayo watumishi ni lazima tuitafute.

(iv) Mambo ya Kushauri

Ndugu wajumbe, Viongozi na Wageni waalikwa;

Kwa kuhitimisha hotuba yangu naomba sasa nishauri badhi ya mambo ambayo nafikiri ni ya muhimu kwa washiriki wa Kikao hiki cha Baraza lakini pia kwa Watanzania kwa ujumla;

(a) Wajumbe wa Baraza, wajiulize kwa nini wao ni wajumbe wa Baraza na kwa nini wako hapa. Wajumbe na kila mtumishi kila siku ujipima kwa kujiuliza umeifanyia nini MAHAKAMA kusaidia utoaji haki kwa wakati kwa muda wote ambao umekuwa mjumbe wa Baraza au umekuwa mtumishi wa Mahakama?

Ninakumbuka hata Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, mara nyingi amesisitiza sana nafsi safi wakati wote wa utoaji wa haki kwa wakati na kwamba wale wenye haki wasicheleweshewe.

(b) Kwa wadau wetu wa MAHAKAMA ni vyema sana wakatafakari namna ya kujiunga na sisi katika SAFARI YA MAHAKAMA MTANDAO/KIDIJITI katika kuharakisha utoaji

haki, kama ambavyo MAHAKAMA, inaunga mkono SERIKALI YA KIDIJITI.

(c) Takwimu za wananchi wetu ni muhimu sana kwa MAHAKAMA ili kujua pia namna ya kupanga mikakati yake ya miundombinu. Ninatoa rai kwa watumishi wote wa MAHAKAMA, asiwepo hata mmoja ambaye atakosa kuhesabiwa siku ya Sensa tarehe 23 Agosti 2022 kama ambavyo watanzania wote watahesabiwa.

Sambamba na hili barua zetu watumishi zionyeshe anwani ya Makazi yetu na tuhakikishe tunaposajili mashauri tunajumiisha anwani za makazi za wahusika ili kurahisisha mawasiliano baina yao wenyewe na baina yao na Mahakama.

(d) Ugonjwa wa UVIKO-19 bado upo, kwa viwango vinavyobadilika. Mahakama itatimiza wajibu wake katika utoaji haki pale watumishi wanajikinga na janga hili. Imethibitika kabisa pasipo shaka kuwa chanjo imesaidia sana.

Mimi nilichanja siku ya kwanza kabisa zoezi lilipozinduliwa na Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ninaomba sana kwa wale ambao bado hawajachanja mfahamu kuwa huchanji kwa ajili ya mtu mwingine bali kwa

ajili yako mwenyewe na afya ya watumishi wenzako na jamii inayokuzunguka.

Nchi zote duniani hazipokei wageni kutoka nchi nyingine ambao hawajapata chanjo. Ingawa sio lazima kuchanja, ninashauri kuwa ni lazima uwe na sababu ya msingi ambayo wewe mwenyewe umejiridhisha kutochanja.

Mwisho kwa mara nyingine tena nichukue fursa hii kuwashukuru sana waandaaji na wajumbe wote na waalikwa wote ambao tumeshiriki katika kikao hiki muhimu sana. Niendelee kuahidi kuwa ofisi yangu itaendelea nanyi kuifanya Mahakama ya Tanzania Taasisi ya mfano, kama ambavyo tayari tumepata tuzo kutoka Ofisi ya Rais Manejimenti ya Utumishi wa Umma ya kuwa washindi wa pili kwa kusimamia vyema utendaji bora na haki za watumishi. Mafanikio mazuri kama haya yanatokana pia na kuwa na Baraza imara kama hili.

Baada ya kusema haya, sasa natamka rasmi kuwa

‘Mkutano wa Baraza la Wafanyakazi wa Mahakama ya Tanzania umefunguliwa rasmi leo tarehe 29/06/2022’

AHSANTENI KWA KUNISIKILIZA